JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

WILAYA YA NANYUMBU
Anuani ya Simu:NANYUMBU
Simu nambari: 2934120 – 2934121
2934122
Barua Pepe: nanyumbu@mtwara.go.tz
Nukushi: 023 – 2510027

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P. 289,
**NANYUMBU.**

*Unapojibu Tafadhali taja:*

**Kumb Na.** NA.96/402/01/789

24 Januari, 2026

# TANGAZO LA JKT

**OFISI YA MKUU WA WILAYA NANYUMBU INAWATANGAZIA NAFASI ZA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) KWA MWAKA 2025/2026**

**Mwombaji awe na sifa zifuatazo:**

1. Awe raia wa Tanzania
2. Umri
   a) Kwa vijana wenye elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18. Waliomaliza Elimu ya Msingi kuanzia Mwaka 2022, 2023, 2024,25 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi.

   b) Vijana wenye elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka 20. Waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka 2022, 2023, 2024,25 na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (***Secondary Leaving Certificate***) na awe na cheti halisi cha matokeo (***Academic Certificate***). Awe na ufaulu wa Daraja la kwanza hadi Daraja la Nne. Kijana mwenye Daraja la Nne awe na ufaulu wa alama kuanzia 26 hadi 32.

CamScanner

c) Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22. Waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka 2022, 2023, 2024,25 na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (***Secondary Leaving Certificate***) na cheti halisi cha matokeo (***Academic Certificate***). Awe na ufaulu wa Daraja la kwanza hadi Daraja la Nne.

d) Vijana wenye elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25. Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

e) Vijana wenye elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26. Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

f) Vijana wenye elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 27. Awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.

3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yeyote ya michoro mwilini (**Tattoo**).

4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.

5. Awe na kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).

7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.

8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa kundi la kujitolea na kundi la lazima (Mujibu wa Sheria).

9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.

10. **Angalizo:** Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za Kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

CamScanner

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

1. Mwisho wa kutuma maombi hayo ni Jumapili tarehe **01/02/2026.**

2. Barua zote zipitishwe na Watendaji wa Kata/Kijiji husika.

3. Muda wa kupokea maombi ni kuanzia saa **1:30 Asubuhi** hadi saa **9:30 Alasiri.**

4. Usaili utafanyika siku ya Jumanne tarehe **03/02/2026** kuanzia **saa 3:00 Asubuhi** katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

**Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 289,
**NANYUMBU.**

Juma S. Kanyinda

**KATIBU TAWALA WA WILAYA**

**24/01/2026**

KATIBU TAWALA WILAYA
NANYUMBU

CamScanner